**HOTUBA YA MAKAMU MKUU WA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA, PROF. ELIFAS T. BISANDA, KWA WAFANYAKAZI WA CHUO ALIYOITOA KWENYE MAKAO MAKUU YA CHUO, TAREHE 4 FEBRUARI 2022.**

***Ndugu Mwenyekiti,***

***Manaibu Makamu Wakuu wa Chuo,***

***Wakuu wa Vitivo,***

***Wakurugenzi,***

***Wakuu wa Vitengo na Idara mbalimbali,***

***Wafanyakazi wote,***

***Mabibi na Mabwana,***

***Habari za Mchana !***

***Nawasalimu kwa jina la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania***

***Ndugu Wafanyakazi wa CKHT***

Nianze kwa kuwatakieni heri na baraka ya mwaka mpya wa 2022. Hiki ni kikao chetu cha kwanza na natumanini sijachelewa. Tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuvuka na kuingia mwaka huu. Tumependelewa, kwani wapo wengi ambao hawakubahatika kama sisi.Wengine wameuona, lakini mara wametoweka.

Tunakumbuka tarehe 20 January tulikusanyika hapa kumwaga mwenzetu, Mwalimu Mdonya Nkerego. Naamini wapo watu wengine, wakiwemo wanafunzi wetu, ambao wamefariki tangu tulipokuwa na kika cha mwisho hapa. Namkumbuka pia Mwalimu Mwakasungula wa FBM, aliyefariki tarehe 9 Novemba, 2021. Kwa heshima yao wote waliofariki, nawaombe tusimame kwa dakika moja kuwaombolezea.

Ndugu Wafanyakazi

Chuo kimeendelea kutekeleza Hati Idhini yake ya (2007) na Sheria ya Vyuo Vikuu Tanzania Na. 7 ya mwaka 2005 kama inavyopaswa katika usimamizi wa vikao vyote vya chuo, masuala ya ufundishaji, utafiti, machapisho, ushauri, ajira na huduma kwa jamii.

Vikao vingi vya kamati za Baraza vilifanyika kama ilivyopangwa, kwa kutumia mtandao wa Zoom.

Mahafali ya 40 yalifanyika visiwani Zanzibar, tarehe 25 Novemba, 2021, kwa ufanisi mkubwa na tuliitumia fursa hiyo kukitangaza chuo huko visiwani. Mpaka sasa hakuna mkoa ulioleta maombi ya kuwa wenyeji wa Mahafali ya 41, na ifikapo kikao cha Baraza la Chuo lijalo, March 25, 2022, tutatangaza kuyafanyia Bungo, Kibaha.

Kazi ya ujenzi wa vituo vitano, huko Manyara, Geita, Simiyu, Lindi na Kigoma karibu imekamilika. Katika kituo cha Kigoma kulikuwa na uchelewaji tokana na kupanda sana vifaa vya ujenzi, hasa saruji, na makosa ya fundi aliyeweka vibaya floor tiles. Naamini sasa kazi za mwisho zitakamilishwa. Tayari watumishi na wanafunzi wa CKHT wanatumia majengo mapya katika vituo vingine, na tunasubiri kukamilisha kazi za nje ili kwa pamoja, majengo yote yazinduliwe. Tunapanga kutumia mfumo wa zoom katika uzinduzi huo, ambao utafanywa na mojawapo ya viongozi wetu wa kitaifa.

Chuo kinakamilisha ukarabati mkubwa wa jengo la Kituo cha Zanzibar, ambao umegharimu karibu Sh Milioni 90 kwa kutumia mapato yetu ya ndani.

## MRADI WA HEET

Chuo kimejiandaa kutekeleza mradi wa HEET, mara fedha itakapotolewa. Mradi huo ni pamoja na ujenzi wa maabara saba za Sayansi katika Kanda saba ikiwemo; Pwani, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Mtwara na Kigoma. Mradi huo pia utakuwa na fedha kwa ajili ya mafunzo, na programu ya Foundation kwa wasichana wanaotarajia kusoma sayansi. Pia kuna fedha imetengwa kwa ajili ya scholarship za Masters na PhD katika maeneo husika.

MKATABA WA KUUNDA BARAZA LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Kuunda Baraza la Wafanyakazi baina ya Menejimenti na chama cha Wafanyakazi uko tayari na umekwisha tiwa Sahihi na wahusika wote. Tayari chaguzi katika vituo vya mikoa zimefanyika, na tunajiandaa kufanya uchaguzi na mikutano katika kanda tarehe 22 Februari, 2022. THTU Pamoja na Menejiment wanapaswa kuangalia chaguzi hizo, ambazo zitasimamiwa na Ofisi ya Kamishina wa Kazi. Tarehe 25 Februari, kutakuwa na Kikao cha Kamati Tendaji ambacho kitafanyikia hapa makao Makuu. Kikao cha Baraza Kuu (Master Workers Council) kimepangwa kufanyika tarehe 18 March, 2022, hapa makao makuu. Hii ni kwa sababu za kifedha, ambao bajeti ya kufanyia kikao Manyara ni kubwa mno, kuliko fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya mwaka huu, na chuo kina uhaba wa fedha kutokana udahili mdogo na shughuli nyingi za kitaaluma kama Mitihani na TP, na vikao vya Baraza na Kamati zake, vyote kuhitaji fedha nyingi.

**MAAMUZI MBALIMBALI YALIYOFANYWA NA BARAZA LA CHUO**.

Ndugu wafanyakazi

Tarehe 19 Novemba 2021, Baraza la Chuo lilifanya kikao chake cha 110 hapa makao makuu. Baraza hilo lilipitisha uteuzi wa wakurugenzi wa mikoa miwili kwa kipindi cha kwanza, ambao ni Dr Nangware Kajia Msofe, Mkoa wa Arusha; na Ndugu Dennis John Semiono, Mkoa wa Kilimanjaro. Kikao pili kiliidhinisha muhula wa pili na wa mwisho kwa wakurugenzi wafuatao: Nd. Ally Abdu (Geita); Nd. Oscar Damas (Kahama); Bi Neema Paul Magambo (Lindi); Dr Ancyfrida Prosper Tibilengwa (Mwanza); Nd. Nassoro Suleiman (Pemba); Dr Julius Frank (Ruvuma) na Nd. Raphael Mokoki (Simiyu).

**MAMBO MTAMBUKA**

CKHT kinajishughulisha katika kuisaidia jamii katika Nyanja mbali mbali. Hivi karibuni, chuo kilitoa madawati na viti chakavu vilivyokuwa vimehifadhiwa kule Bungo Kibaha, vikakarabatiwa na kugawiwa shule mbalimbali katika mkoa wa Pwani.

Katika kuadhimisha siku ya wanawake tarehe 8 Machi, 2022, Tawi la THTU Wanawake la CKHT, limekusudia kupeleka vifaa mbali mbali kwa wagojwa wa Saratani katika hospitali za Muhimbili na Ocean Road. Vifaa vinavyokusanywa ni Pamoja na colostomy bags, sabuni, mafuta ya kujipaka, dawa za meno, kandambili, Pampas za Watoto, Miswaki, Maziwa ya unga, khanga na vitenge, Pampas za wakubwa, Napkin tissue,

wipes, n.k. Jumla ya bajeti inayohitajika ni Sh 4,075,000. Kutokana na uhaba wa fedha chuoni, Chuo kitachangia sh 2,000,000. Tunawaomba wafanyakazi wote, tuwaunge mkona akinamama wetu, ili tupate 2,075,000= zilizosalia. Namruhusu Stella Shayo aanze sasa kuchangisha kiasi hicho au Zaidi. Tuwakumbuke wenzetu walio katika shida, na maumivu kwenye hospitali zetu.

## ZIARA YA KITALII

Chuo kimetoa idhini ya wafanyakazi kuandaa ziara ya utalii wa ndani katika mbuga zetu za Wanyama za Tarangire, Serengeti, Ngorongoro na kisiwa cha Saa nane kule Mwanza, Mwezi Julai mwaka huu. Gharama ya kushiriki ni Sh 500,000 kwa mtu mmoja. Mzunguko wote utakuwa siku saba (7). Kuna nafasi 22 tu, hivyo atayewahi ndiye atasajiliwa. Wale mnaopenda kushiriki ziara hii mnashauriwa kujiandikisha na kulipia michango yenu kwa Sarah Abdi au Thereza Bagenda.

***Ndugu Wafanyakazi***

Kuanzia mwaka huu wa fedha, chuo chetu kimepewa muundo mpya (Organizational Structure). Baadhi ya vitengo vimeondolewa au kuunganishwa na vitengo vingine. Idara za kitaaluma ndizo tu zinatambulika, katika muundo mpya, ambapo nazo zimepunguzwa katika vitivo vyote.

## MUUNDO MPYA

**A. Office of Deputy Vice Chancellor – (Academic, Research and Consultancy)**

(i) Faculty of Arts and Social Sciences;
(ii) Faculty of Business Management;
(iii) Faculty of Education;
(iv) Faculty of Law;
(v) Faculty of Science, Technology and Environmental Studies;
(vi) Institute of Continuing Education;
(vii) Teaching, Learning and Examination Services Directorate;
(viii) Research, Publication and Innovation Directorate;
(ix) Postgraduate Studies Directorate;

(x) Undergraduate Studies Directorate; and
(xi) Consultancy Services Directorate.

**B. Office of Deputy Vice Chancellor – (Planning, Finance and Administration)**

(i) Human Resource Management and Administration Directorate;
(ii) Finance and Accounts Directorate;
(iii) Planning and Development Directorate; and
(iv) Students' Services Directorate

**C. Office of Deputy Vice Chancellor – (Learning Technologies and Regional Services)**

(i) Library Services Directorate;
(ii) Institute of Educational and Management Technologies;
(iii) Regional Centres;

**OFFICE OF THE VICE CHANCELLOR**

D. Communication and Marketing Unit;
E. Quality Assurance Unit;
F. Internationalization and Convocation Unit;
G. Legal Services Unit;
H. Internal Audit Unit; and
I. Procurement Management Unit.

Ili tuanze kutekeleza muundo mpya wa utawala, kuanzia sasa nimetengua uteuzi wa wakuu wote wa idara. Pia ninatengua uteuzi wa Wativa washirika (Associate Deans) wa Wakurugenzi washiriki (Associate Directors), ambapo nafasi hizo zimeondolewa katika muundo mpya. Naomba sasa nitangaze wakuu wa idara katika muundo mpya katika vitivo vyetu.

OCB kuanzia sasa ni kitengo kinachojitegemea, na kitaajiiri na kulipa wafanyakazi wake, chini ya Bodi ya OCB ambayo nayo itaundwa upya. Kutakuwa na Mkurugezi wa Ushauri wa Kitaalam, ambaye atakuwa chini ya DVC Academic, na atakuwa pia mjumbe wa Bodi ya OCB. Policy ya Consultancy inapaswa kuzingatia marekebisho haya.

| FACULTY | DEPARTMENT | FAVOURED |
|---|---|---|
| FASS | Economics and Community Economic Development(ECED) | **Dr Emmanuel Nyankweli** |
| | Sociology and Social Work(SOSW) | **Dr Mariana Makuu** |
| | Political Science, Public administration, History, and Philosophy(PSPA) | **Dr Jacob Lisakafu** |
| | Languages and Literary Studies(LLS) | **Dr Dunlop Ochieng** |
| | Geography, Tourism and Hospitality services(GHTH) | **Dr Halima Kilungu** |
| | Media studies and Library Services(MLS) | **Dr Henry Mambo** |
| | | |
| FBM | Accounting and Finace | **Dr Saganga Kapaya** |
| | Marketing, Entrepreneurship and Management | **Dr France Shayo** |
| | | |
| FED | Psychology and Special Education | **Innocent Messo** |
| | Education Foundations, Adult and Distance Education | **Dr Zamzam Nyandara** |
| | Curriculum and Instructions | **Dr Jesse Lukindo** |
| | Education Policy, Planning and Administration | **Dr Winfrida Malingumu** |
| | | |
| FLW | Private Law | **Dr Doreen Mwamlangala** |
| | Public Law | **Ms Mbiki Msumi** |
| | | |
| FSTES | Physical and Environmental Sciences | **Dr Paul Ikwaba** |
| | Mathematics and ICT | **Dr Rogers Bhalalusesa** |
| | Biological and Food Sciences | **Dr Happy Magoha** |
| | | |

Pia, Mratibu wa IGU, kuanzia sasa atakuwa Ndugu Richard Laizer, kutoka FBM, anayechukua nafasi ya Dr Proches Ngatuni.

Katika Mabadiliko ya Muundo, kitengo cha UTLS kinapelekwa kurugenzi ya Mitihani. Kurugenzi ya Mipango na Maendeleo itakuwa chini ya DVC RM. Tunararajia kubadili muundo katika kurugenzi nyingine na vitengo. Nafasi zitakazokuwa wazi zitatangazwa hapo baadaye baada ya kuridhia miundo mipya.

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza, KAZI IENDELEE.